Usipopiga kura unatoa nafasi wachache kujiamulia kwa urahisi zaidi na kufanikiwa.

Sisi Empowering Lives Together Foundation tunapenda kusisitiza watanzania tufikirie vizuri juu ya umuhimu wa kila mwenye sifa kushiriki kupiga kura kwenye Uchaguzi Mkuu siku ya Jumatano, tarehe **28/10/2020** bila kujali changamoto tulizonazo. Katika hali fulani namna pekee ya kuelewa jambo ni kupitia kuelewa ukinyume wa jambo hilo. Hivyo kama itatusumbua kuelewa umuhimu wa kupiga kura basi tujaribu kutafakari ubaya wa kutokupiga kura na kama hatuelewi ubaya wa kusema wengine watapiga kwa niaba yetu hebu tufikiri ikiwa wengine watafikiri vivyo hivyo matakeo yatakuwaje katika jamii?

**Hivyo mtu yoyote anapaswa kupiga kura kwa sababu:-**

**1. Haki yake na ni wajibu pia.**
Kila mtanzania ana haki na wajibu wa kupiga kura na kumchagua kiongozi anayeona anafaa kwa maendeleo ya nchi.

**2. Kuthaminiwa mawazo yake.**
Kupiga kura ni njia mojawapo ya kuwasilisha mawazo yako kuwa unaona kiongozi yupi anafaa kuongoza jamii ambayo ameomba kuiongoza hivyo unavyopiga kura unawasilisha mawazo yako.

**3. Kuchagua kiongozi anayefaa.**
Unapopiga kura unachagua kiongozi unayeona anafaa. Hivyo kushiriki kupiga kura katika uchaguzi ni muhimu sana.


**4. Kupeleka ujumbe.**
Mwananchi anapopiga kura anapeleka ujumbe kuwa kiongozi yupi anafaa hivyo anasaidia jamii na wenye mamlaka kujua kiongozi yupi ni mzuri na anafaa kwa maendeleo ya wananchi.

**5. Kura ni sauti yako.**
Unapopiga kura ndipo unafikisha ujumbe wa namna gani unataka uongozwe au unahitaji uongozi wa aina gani hivyo kura yako inauwezo wa kukuletea mabadiliko chanya. Kupiga kura ni haki ya kila mtu, hivyo kila mwenye sifa anastahili kupiga kura haijalishi changamoto alizonazo. Empowering Lives Together Foundation inawahamasisha watanzania wote wenye sifa na waliojiandikisha kwenda kupiga kura kuchagua Rais, Wabunge na Madiwani kwenye Uchaguzi Mkuu unaofanyika siku ya Jumatano, tarehe 28/10/2020.

**"WATANZANIA WOTE WENYE SIFA ZA KUPIGA KURA TUKAPIGE KURA"**







## "TWENDE TUKAPIGE KURA"

### Contact Us


**ADDRESS**
Apartment No. 309 Situated on
Plot No. 459-1533/159,
Nkrumah Street, Ilala Municipality,
Dar es salaam, Tanzania.

**CALL/E-MAIL**
Phone: +255 692 899 662
Email: info@eltf.or.tz

EMPOWERING LIVES TOGETHER FOUNDATION
JOIN HANDS FOR INCLUSION

# ELIMU KWA MPIGA KURA UCHAGUZI MKUU 2020





## ELIMU KWA MPIGA KURA UCHAGUZI MKUU 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kutelekeza majukumu yake ya kikatiba, mwaka huu 2020 inaratibu na kusimamia uendeshaji wa Uchaguzi wa Rais, Wabunge katika Jamhuri ya Muungano na Uchaguzi wa Madiwani kwa Tanzania Bara. Kupitia Kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, inatoa Elimu kwa Mpiga Kura lakini pia imetoa vibali kwa Asasi mbalimbali kutoa Elimu kwa Mpiga Kura ambayo ni kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi juu ya mambo ya msingi yatakayo wawezesha kutekeleza kwa usahihi jukumu la kupiga kura Siku ya Uchaguzi Mkuu ambayo ni siku ya Jumatano, tarehe 28 Oktoba, 2020.

Yafuatayo ni mambo ya msingi yanayopaswa kufahamika kwa Mpiga Kura: -

### 1. Nani anaruhusiwa kupiga kura?

Mtu anayeruhusiwa kupiga kura ni yule mwenye sifa zifuatazo:

(i) Raia yeyote wa Tanzania aliyeandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na ana kadi ya kupiga kura iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi; na

(ii) Awe ni mkazi wa kawaida wa eneo analotaka kupigia kura au amehamia na taarifa zake zimehamishiwa katika kituo anachotaka kupiga kura.

### 2. Wapi unaweza kupiga kura?

Kituo utakachopigia kura ni kile ulichotumia kujiandikisha na kupata kadi yako ya kupigia kura na mahali ambapo jina lako litaonekana. Tume itabandika orodha ya wapiga kura kituoni siku 8 kabla ya siku ya uchaguzi. Ili uweze kujua kilipo kituo chako cha kupigia kura unaweza kutumia simu yako ya mkononi kwa kupiga namba *152*00# kisha chagua Uchaguzi Mkuu na fuata maelekezo au piga simu namba 0800112100 (Bure) ambayo ni huduma kwa Mpiga Kura. Aidha, Makarani waongozaji watakuwepo katika vituo vya kupigia kura kuwasaidia wapiga kura kutambua vituo vyao.

### 3. Kituo cha kupigia kura

Kituo cha kupigia kura kitabandikwa bango jeupe lililoandikwa KITUO CHA KUPIGIA KURA na nje ya kituo kutabandikwa mabango yanayotoa Elimu ya Mpiga kura.

### 4. Muda wa kupiga kura

Siku ya uchaguzi vituo vya kupigia kura vitafunguliwa saa moja kamili asubuhi na kufungwa saa kumi kamili jioni kwa Tanzania Bara. Kwa Tanzania Zanzibar, vituo vitafunguliwa saa moja kamili asubuhi na kufungwa saa kumi na moja kamili jioni.

Mambo muhimu ya kuzingatia

(i) Mpiga Kura anatakiwa kufika kituoni katika muda uliotanganzwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi;

(ii) Muda wa kupiga kura ukiisha hakuna mtu mwingine yeyote atakayeruhusiwa kupiga kura; kama muda ukiisha na wapiga kura bado wapo kwenye mstari, Askari wa kituo atasimama nyuma ya mtu wa mwisho mpaka wote wamalize zoezi la kupiga kura;

(iii) Mpiga Kura anatakiwa kutunza kadi yake na kuitumia kwa ajili ya kupiga kura tu;

(iv) Siku ya Uchaguzi Mpiga Kura hatakiwi kuvaa nguo zinazoashiria itikadi ya chama chochote cha siasa;

(v) Watu wenye ulemavu, mama wajawazito na wenye watoto wachanga walioenda nao kituoni, wazee na wagonjwa watapewa kipaumbele; na

(vi) Ikiwa jina lako haulioni katika Orodha ya Wapiga kura kituoni, mpiga kura anatakiwa amuone Karani Mwongozaji wapiga kura (Direction Clerk) ili akusaidie kupata maelekezo au kukuonyesha kituo chako cha kupiga kura.

### 5. Kabla ya kupiga kura

Kabla ya kuanza kupiga kura Msimamizi wa kituo atafungua masanduku ya kuhifadhia kura na kuwaonyesha Mawakala wote na watu wengine wanaohusika na Uchaguzi waliopo katika kituo. Masanduku ya kuhifadhia kura yatafungwa na kuwekewa lakiri (seal), baada ya hapo yatawekwa mahali pa wazi wakati wote wa upigaji kura.

Msimamizi wa Kituo pia ataonyesha bahasha yenye karatasi za kupigia kura ambazo vimefungwa kuonyesha kuwa hakuna mtu aliyezifungua hapo kabla.

### 6. Jinsi ya kupiga kura

(i) Mpiga kura atamkabidhi Msimamizi wa kituo kadi yake ya kupiga kura;

(ii) Jina la Mpiga Kura litasomwa kwa sauti kubwa ili Mawakala wa Vyama waliopo wasikie;

(iii) Msimamizi wa Kituo na Mawakala wa Vyama vya siasa wakiwa na shaka wana haki ya kuuliza maswali ili wajiridhishe;

(iv) Msimamizi wa Kituo atamkabidhi Mpiga Kura karatasi ya kura ya aina 1 ya Rais au 2 za Ubunge na Udiwani au 3 za Rais, Ubunge na Udiwani na pia atamuonesha jinsi ya kukunja karatasi hizo;

(v) Mpiga Kura ataenda sehemu maalumu iliyotengwa kwa ajili ya kupiga kura;

(vi) Mpiga Kura ataweka alama ya vema (√) ndani ya chumba kilichopo mbele ya picha ya mgombea anaemtaka;

(vii) Mpiga Kura atatumbukiza karatasi zake za kura katika masanduku kwa jinsi atakavyoelekezwa;

(viii) Kabla ya kuondoka kituoni, Mpiga Kura atachovya kidole chake kidogo cha mkono wa kushoto katika wino maalumu usiofutika.

### KURA YAKO, SAUTI YAKO, NENDA UKAPIGE KURA

Kwa kuwa binadamu tunaishi katika jamii ni muhimu kila mwanadamu kushiriki katika ustawi wa jamii kwani jamii inapostawi ndio pia ustawi wa mtu mmoja mmoja unatokea na kuendelea. Na kwa kuwa katika jamii kuna uongozi ambao ndio unaoendesha gurudumu la maendeleo ya jamii husika basi kila mtu mwenye sifa stahiki ana wajibu wa kushiriki kuchangua uongozi katika jamii husika kwani uchaguzi ni sehemu kuu ya michakato ya kidemokrasia duniani kote. Pamoja na changamoto mbalimbali lakini umuhimu wa watu kupiga kura unabaki kuwa palepale maana wengine hutoa visingizio mbalimbali kama ulemavu, foleni, kutokuwa na vifaa vya kuwawezesha kupiga kura n.k. Tunaomba kusisitiza kwamba kuacha kupiga kura sio suluhisho la changamoto hizo bali linaongeza matatizo mengine zaidi. Hivi fikiria usipopiga kura bila sababu za msingi na wengine wakakuwakilisha katika kuchagua viongozi, basi hebu fikiria kwa makini na kujiuliza wakati wa kulalamika pale uongozi ambao hukutaka kushiriki kuchagua unapoenda kinyume na matakwa yetu tunajisikiaje? Je utamlaumu nani? Utasema wamekuchagulia kiongozi asiyefaa? Je malalamiko yetu yanapata msingi au uhalali upi ikiwa haukupiga kura? Je tunaelewa nini kuhusu uhuru na wajibu? Kama tunatumia uhuru wetu kutokuchagua basi tuanze kuelewa kuwa kwa kufanya hivyo tunapoteza haki ya kulalamika dhidi ya utawala ambao hakutushiriki kwa makusudi kuuweka.